

Maswali

1. Kufufuka kwa Yesu kulithahirisha ninI?
2. Kando na kufufuka kwake kulikuwa na matokea gani tena?
3. Wanafunzi walifanya nini kuonyesha kwamba maneno y a Yesu yalikuwa na umuhimu?
4. Mbona watu walifurahia Anania na Safira?
5. Anania alikosa nini?
6. Safira alikosa nini?
7. Tunajifunza nini kwa hadithi hii ya huzuni?

Majibu

1. Kulithahirisha yeye ni Mwana wa Mungu.
2. Maneno ya Yesu yalikuwa na matokeo makubwa kwa wanafunzi wake.
3. Waliokuwa na vitu au nyumba walitumia wote au waliuza. Walipeana pesa kulisha na kuvaa maskini.
4. Kwa sababu waliuza nyumba na kuletea maskini pesa.
5. Alidanganya. Alisema aliletea Petro pesa zote kutoka kwa mauzo lakini alikuwa ameficha zingine.
6. Naye pia alidanganya.
7. Ni lazima tumwamini Mungu kabisa kwa kila kitu. Tena lazima tuwa waaminifu na tuiseme uongo.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 2



46 Anania na Safira

Marejeo

Matendo ya Mitume 5:1-10

Kiini cha somo

Hatuwezi kudanganya Mungu. Mungu atatulinda.

Maneno maalum

1. Mzima + Mwana wa Mungu + mbinguni
2. Zungumza + matokeo + maskini
3. Mali + uza na kugawana + Petro + kujitolea.
4. Anania na Safira + uza + jihisi vizuri.
5. Jibu la Anania + danganya + kufa.
6. Soma + uaminifu + amini Mungu.

46.1 Hebu fikiria furaha yenye rafiki wa Yesu, yaani wanafunzi waliyokuwa nayo baada ya kujua kwamba amerudi kutoka kwa wafu. Alikuwa amefufuliwa kutoka kwa wafu. Alikuwa yu hai na mzima. Kufufuka kwa Yesu kulikuwa thahirisho kwamba yeye ni Mwana wa Mungu. Yesu alikaa na marafiki wake kwa juma chache baada ya kufufuka. Baadaye alitoka hapa duniani kuenda kuishi mbinguni na Mungu Baba yake. Hata sasa ako huko.

46.2 Baadaye marafiki wa Yesu walienda kukaa pamoja. Walizungumzia maneno yenye Yesu alisema na kutenda. Mafundisho ya Yesu yalikuwa na matokeo makuu kwa wanafunzi wake. Walijali wenzao waliokuwa maskini. Hakuna aliyekuwa na njaa.

46.3 Wanafunzi waliokuwa na pesa nyingi waliletea Petro ili anunulie chakula na nguo. Alikuwa ndiye mweka hazina na aliweka mpangilio wa matumizi ya hizo pesa. Baadhi ya watu waliuza vitu vyenye hawakuhitaji tena. Waliletea Petro pesa ya mauzo yao. Wengine waliishi na wenzao wenye hawakukuwa na makao. Hakuna aliyelazimishwa kufanya lolote. Walikuwa na uhuru wakufanya walichotaka.



46.4 Anania na Safira walikuwa na nyumba nzuri. Haikuwa kubwa ya kukaa na wenzao. Kwa hivyo waliuza na kuletea Petro pesa. Kila mtu alifurahia hicho kitendo. Lakini Anania hakuletea Petro pesa zote.



46.5 Baada ya siku chache, Petro alienda kuona Anania na akamuuliza, “Anania, ulinipa pesa zote ulizopata kwa mauzo?” Anania alijibu, “Ndio.” Alikuwa anadanganya. Petro akamwambia, “Ninajua kwamba pesa ulizoleta sio zote. Haikukuwa makosa wewe kujiwekea pesa zingine. Ilikuwa makosa kusema umeniletea pesa zote ili uonekane mzuri mbele ya watu. Umetudanganya sisi pamoja na Mungu.” Anania aliposikia hayo, alizirai na akafa.

46.6 Baada ya mda mfupi, Safira alirejea. Hakuja kilichokuwa kimetendeka kwa mmewe. Petro alimuuliza, “Mliletea pesa zote baada ya kuuza nyumba.” Safira alijibu, “Ee ndiyo. Nimekwambia ukweli.” Petro alihuzunika sana na kusema, “Nijambo mbaya sana wewe na mmeo mlimpanga kufanya. Walioenda kuzika mmeo hawajarudi. Sasa watazika wewe pia.” Safira aliposikia hayo alizirai na akafa.

46.7 Hii ni hadithi ya huzuni sana. Makosa ya Anania na Safira ina somo linalotupasa tujifunze. Hawakukuwa waaminifu. Walidanganya ndugu dada, na hata Mungu. Haikukuwa makosa kujiwekea pesa zingine lakini makosa ni kujifanya kwamba hawakuweka. Na labda hawakuamini kwamba Mungu anaweza kuwapa vitu vingine vyenye watahitaji. Labda hii ilifanya wakaficha pesa zingine. Mungu anataka tumwamini kabisa. Hatuwezi kutarajia vitu vizuri kutoka kwa hii dunia ya Mungu na hali tunataka tupate kutokana na maisha ya ulimwengu.

